
# Mwelekeo wa Msimu wa Mvua kwa Ngazi ya Mkoa na Wilaya zake

**MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2023 KWA MKOA WA MJINI MAGHARIBI, UNGUJA**
**Umetolewa: 22/02/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2023; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika mkoa wa Mjini Magharibi na wilaya zake.

### (I) Ngazi ya Mkoa




**Kielelezo 1: (a)** Mwelekeo wa msimu wa Masika, 2023 kwa kisiwa cha Unguja. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Masika katika sehemu mbalimbali za kisiwa cha Unguja. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Machi hadi Mei, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

### Dondoo

- *Kwa ujumla mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi, 2023.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Juni, 2023.*
- *Vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa kujitokeza hususan katika mwezi Aprili, 2023.*

### Mvua za msimu wa Masika, 2023

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi, 2023 na kuisha Juni, 2023.

***Angalizo:***
*Izingatiwe kuwa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani hivyo matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa zinazoambatana na upepo mkali yanatarajiwa kujitokeza.*

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz




**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

(II) Ngazi ya Wilaya

**MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2023 KWA WILAYA YA MAGHARIBI**
**Umetolewa: 22/02/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2023; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Magharibi.




Mwelekeo wa mvua za Masika Machi-Mei, 2023 kwa wilaya ya Magharibi, Unguja.

**Dondoo muhimu**

- *Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Magharibi.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya tatu ya mwezi Machi, 2023.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Juni, 2023.*
- *Uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua na uhifadhi wa malisho kwa matumizi ya baadae.*

**Mvua za Msimu wa Masika, 2023 kwa Wilaya ya Magharibi**

**Zitaanza:** Wiki ya tatu ya mwezi Machi, 2023.

**Zitaisha:** Mwezi Juni, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Magharibi ni kati ya milimita 490 hadi 940.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Mei, 2023.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku 10 au zaidi hususan mwezi Aprili katika msimu huu wa Masika, 2023.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa za kuridhisha na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.

**Angalizo:**

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

**Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi**
**Matokeo**

- Hali ya unyevu wa udongo kwa ustawi wa mazao ya chakula, biashara na matunda yakiwemo mpunga, migomba, mahindi, mtama, karafuu, nazi na michungwa inatarajiwa kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi.
- Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao hasa wakati wa msimu wa mvua yanaweza kujitokeza.
- Uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha.

**Ushauri**

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wavuvi wanashauriwa kuandaa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya uvuvi pamoja na kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**


727N – 00/2023

# Mwelekeo wa Msimu wa Mvua kwa Ngazi ya Mkoa na Wilaya zake

(II) Ngazi ya Wilaya

**MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2023 KWA WILAYA YA MJINI**
**Umetolewa: 22/02/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2023; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Mjini.




Mwelekeo wa mvua za Masika Machi-Mei, 2023 kwa wilaya ya Mjini, Unguja.

**Dondoo muhimu**

- *Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Mjini.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya tatu ya mwezi Machi, 2023.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Juni, 2023.*
- *Uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua na uhifadhi wa malisho kwa matumizi ya baadae.*

**Mvua za Msimu wa Masika, 2023 kwa Wilaya ya Mjini**

**Zitaanza:** Wiki ya tatu ya mwezi Machi, 2023.

**Zitaisha:** Mwezi Juni, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Mjini ni kati ya milimita 490 hadi 680.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Mei, 2023.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku 10 au zaidi hususan mwezi Aprili katika msimu huu wa Masika, 2023.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa za kuridhisha na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.

**Angalizo:**

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

**Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi**
**Matokeo**

- Hali ya unyevu wa udongo kwa ustawi wa mazao ya chakula, biashara na matunda yakiwemo mpunga, migomba, mahindi, mtama, karafuu, nazi na michungwa inatarajiwa kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi.
- Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao hasa wakati wa msimu wa mvua yanaweza kujitokeza.
- Uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha.

**Ushauri**

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wavuvi wanashauriwa kuandaa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya uvuvi pamoja na kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz



**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

727N – 00/2023